# CHATO yetu

TOLEO NAMBA 17 JANUARI HADI MACHI 2019

LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA HABARI NA UHUSIANO CHA HALMASHAURI WA WILAYA YA CHATO www.chatodc.go.tz Email: ded@chatodc.go.tz


## Miradi ya Kimkakati Kuongeza Kiwango cha Mapato ya Ndani ya Halmashauri




## Vikundi Vyanufaika na Mikopo ya 10%

Uk.11



Uk.2



## Baraza Lapitisha Bajeti ya Shilingi Bilioni 49

UK. 2

## Miradi ya Kimkakati Kuongeza Kiwango cha Mapato ya Ndani

Halmashauri ya Wilaya ya Chato katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwenye vipaumbele vyake ilipanga kuanzisha miradi mipya ya kwa lengo la kuongeza kiwango chake cha mapato ya ndani ili kuweza lukidhi matarajio yake ya utoaji wa huduma kwa wananchi.

Kupitia maandiko mbalimbali yalipelekwa Ofisi ya Rais–TAMISEMI timu ya Menejimenti ya Halmashauri ili ainisha miradi kadhaa ikiwemo viwanda vikubwa na vya kati ili kuongeza uwezo wa Halmashauri kujitegemea kiichumi.

Miradi ambayo ilifanikiwa na kupata fedha ni kiwanda cha ufatuaji wa Matofali kilichopo kijiji cha Muungano na Uchapishaji uliopo kijiji cha Kitela kata ya Chato.

Jumla ya fedha iliyotolewa kwa miradi hii miwili ilikuwa ni shilingi 305,712,110.

Kupitia miradi mipya hiyo ambayo imeanza uzalishaji tangu mwezi Machi 2019 Halmashauri ya Wilaya ya Chato inaelekea kupata ufumbuzi wa tatizo la muda mrefu la utoshelevu wa mapato ya ndani ya Halmashauri.

Mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri ikupia vyanzo vya ndani hadi kufikia mwezi Juni 2018 ilikusanya kiasi cha shilingi 1,956,905,535.45 sawa na 90.65% ya lengo la 2,158,800,000.

Kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia tarehe 31 Machi 2019 Halmashauri kupitia vyanzo vya ndani imekusanya kiasi cha shilingi 1,572,278,292.09 Sawa na 69.36% ya lengo la shilingi 2,266,934,000.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato Eliurd Mwaiteleke amesema kuanza kwa miradi hiyo ni dalili ya kwamba kwa mwaka 2018/2019 mapato yatakuwa ni zaidi ya asilimia 100.

"Pamoja na vyanzo vingine vya Halmashauri lakini kupitia miradi hii ya kimakakati tunatarajia makusanyo yetu ya ndani yatakuwa ni zaidi ya mwaka uliopita kwa kiwango kikubwa tu" alisema Mkurugenzi Mtendaji.

Kwa mujibu wa meneja wa kiwanda cha matofali George Philipo amesema tofali moja la nchi 6 kwa (uwiano wa mfuko mmoja tofali 40) kwa bei ya kiwandani linauzwa shilingi 1100/=.

## Baraza Lapitisha Bajeti ya Shilingi Bilioni 49

Baraza la madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Chato limepitisha bajeti ya makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2012 ya kiasi cha shilingi 49,869,076,947 ambapo kiasi cha shilingi 2,936,534,000 ni fedha ambazo zinatarajiwa kukusanywa na Halmashauri kutoka kwenye vyanzo vyake mbalimbali vya mapato.

Akiwasilisha taarifa ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2019/2020 Afisa Mipango wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato David Sinyanya amesema bajeti hiyo imelenga kujenga uwezo wa kiutawala katika maeneo yote, pamoja na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato Mhe. Christian Manunga amesema ni vyema katika bajeti hii Halmashauri ikajikita zaidi katika ukusanyaji wa Mapato pamoja na kukamilisha maboma yaliyopo katika maeneo mbalimbali ya vijiji.

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri ilikadiria kukusanya kiasi cha shilingi 52,184,131,192.



# Mawaziri 8 Watua Kutatua Migogoro ya Ardhi Kwenye Hifadhi



Mawaziri 8 wakiongozwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. William Lukuvi wamefika Wilayani Chato kwa lengo la kutatua migogoro ya rdhi katika hifadhi za misitu.

Akitoa taarifa ya Wilaya kwa msafara huo, Mkuu wa Wilaya ya Chato Mhandisi Mtemi Msafiri amesema kwa Wilaya ya Chato kata ya Bwanga, Iparamasa, Butengorumasa, Buziku, Nyarutembo, Kasenga na Bwongera zinao wakazi wengi ambao wanafanya shughuli za kiuchumi katika hifadhi za misitu hiyo ikiwemo kilimo na ufugaji.

Amesema kutokana na ukuaji wa miji inayopakana na hifadhi hususan kata ya Bwanga ni dhahiri kuwa kunahitajika ardhi kubwa kwa ajili ya uendelezaji wa mji huo ikiwemo ujenzi wa taasisi na maeneo ya viwanda.

Akiongea na wananchi waliokusanyika shule ya sekondari Magufuli waziri Lukuvi amesema amesikiliza kero za wananchi wa Chato na Bukombe kuhusiana na uhaba wa ardhi na kuhaidi kufikisha kero hizo kwa mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mawaziri wengine walikuwepo kwenye msafara huo ni pamoja na Waziri wa nchi ofisi ya Rais-TAMISEMI Mhe. Selemani Jafo, Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Hamis Kigwangala, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mhe, Husen Mwinyi, Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Luhaga Mpina, Waziri wa Maji Mhe. Profesa Makame Mbarawa, Naibu waziri wa Kilimo na naibu waziri ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Mazingira.

## Wanufaika TASAF 3 Wajikita Kwenye Ufugaji

Baadhi ya wanufaika wa mpango wa TASAF awamu ya tatu Wilayani Chato wameendelea kujiongezea kipato kwa kufuga aina mbalimbali za mifugo.

Baadhi ya wanufaika wamesema kupitia ufugaji wameona ndio njia pekee ya kwao kujikwamua na hali ngumu ya maisha ambayo walikuwa nayo kabla ya kuingia kwenye mpango wa TASAF 3 wa kunusuru kaya masikini.

Bi Sugwa Bushuwandama mkazi wa kijiji cha Mkungo kata ya Bukome Wilayani hapa anasema kupitia mpango wa TASAF 3 kwa kipato kidogo anachopata hivi sasa anao mbuzi 12 ambao mara kwa mara amekuwa anauza na kununua mahitaji mengine ya familia kama vile chakula.

Kupitia miradi hiyo ya ufugaji wanufaika hao wameomba kutembelewa na wataalamu wa mifugo kwa ajili ya ushauri wa ufugaji bora pamoja na utengenezaji wa mabanda imara kwa ajili ya mifugo yao.

Wilaya ya Chato ina jumla ya wanufaika wa Mpango wa TASAF awamu ya tatu 7,666 Kati yao wanufaika 1000 Wamejikita kwenye miradi ya ufugaji wa mbuzi, Kondoo, kuku, Bata, Nguruwe na Ng'ombe na baadhi wameanzisha biashara ndogo ndogo kama njia ya kujiongezea kipato cha kaya.

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO**

# TANGAZO

**WANANCHI WOTE MNATANGAZIWA KUWA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO IMEANDAA MAENEO YA VIWANJA VIDOGO VYA KUJENGA VIBANDA KATIKA STENDI YA MUGANZA KWA AJILI YA KUJENGEWA MABANDA YANAYOZUNGUKA STENDI YA MABASI KATIKA MJI WA MUGANZA**

**WANANCHI WOTE WENYE NIA YA KUPATIWA VIWANJA VYA KUJENGA VIBANDA HIVYO WANAJULISHWA KUWA KUANZIA TAREHE 01/04/2019 HADI 14/04/2019 FOMU ZA MAOMBI YA VIWANJA VYA KUJENGA VIBANDA HIVYO ZITATOLEWA OFISI ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO KWA GHARAMA YA TSHS 20,000/=**

**WATU WOTE WENYE NIA YA KUPATA VIWANJA VYA KUJENGA VIBANDA KATIKA ENEO LA STENDI MUGANZA WANATAKIWA KUJAZA FOMU HIZO NDANI YA MUDA ULIOONYESHWA KWENYE TANGAZO HILI, NA ENDAPO MWOMBAJI ATAFANIKIWA KUPATA KIWANJA CHA KUJENGA KIBANDA HICHO, ATAPASWA KULIPA TSHS 350,000/= KAMA DHAMANA YA KUPATIWA KIWANJA CHA KUJENGA KIBANDA**

**WATU WOTE WATAKAOFANIKIWA KUPATA VIWANJA VYA KUJENGA VIBANDA VYA STENDI, MARA BAADA YA MALIPO YA DHAMANA WATAPASWA KUJAZA MIKATABA BAINA YAO NA HALMASHAURI YA WILAYA AMBAPO MIKATABA HIYO ITAAMBATANA NA MICHORO NA MASHARTI YA UJENZI WA VIBANDA HIVYO**

**LIMETOLEWA NA ,**
**OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO.**

## SIKU YA WANAWAKE DUNIANI;

## DC Awatahadhalisha Wanafunzi wa Kike kuhusu Mimba

Serikali Wilayani Chato imeonya tabia ya baadhi ya wanafunzi wa kike kuwaficha wanaume wanaowapa ujauzito pindi wanapofikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Onyo hilo limetolewa na Mkuu wa Wilaya ya Chato Mhandisi Mtemi Msafiri kwenye maadhimisho ya siku ya wanawake duniani yaliyofanyika kiwilaya kata ya Nyamirembe.

Mkuu wa Wilaya amesema kumekuwa na tabia ya baadhi ya wanafunzi wa kike kuficha taarifa za waliowapa mimba na kusema kuwa kuanzia sasa serikali itakuwa inawachukulia hatua wenyewe kwani tatizo la mimba mashuleni limekithiri sana.

"*naomba niwatangazie kuanzia sasa wanafunzi wa kike ukipata ujauzito na ukamficha aliyekupa ujauzito au ukimsaidia kutoroka tunakushitaki wewe mwenyewe*" alisisitiza Mkuu wa Wilaya

Katika hatua nyingine Mkuu wa Wilaya ya Chato amewaasa wanawake wote kutoa taarifa juu ya unyanyasaji na unyanyapaa wanaofanyiwa wanawake majumbani na mahali pa kazi. Amewataka wanawake kutoa taarifa kwenye vyombo vya dola hususan TAKUKURU.

Kaulimbiu ya maadhimisho ya siku ya wanawake duniani mwaka 2019 ilikuwa "Badili fikra kufikia usawa wa kijinsia na maendeleo endelevu"



# Vijana Chato Wapata Elimu ya Kilimo cha Kisasa

Zaidi ya Vijana 100 kutoka maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Chato wamenufaika na mafunzo ya kilimo kwa njia ya Kitalu nyumba (Greenhouse ) yanayotolewa na Wizara ya Kazi, Ajira na Walemavu.



Mafunzo hayo yaliyofanyika kwa muda wa siku 8 yanalenga kuwajengea uwezo vijana wa jinsia zote ili waweze kujiendeleza kupitia sekta ya Kilimo.

Akiongea na Afisa Habari wa Halmashauri afisa kilimo anayeshughulika na mradi huo Edgar Kimario amesema vijana hao wamepata mafunzo hayo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa agizo la Wizara husika inayogharamia mafunzo hayo pamoja na ujenzi wa miundombinu ya kujifunzia kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Chato.

Amesema kwa kuanzia vijana hao wamepata elimu ya darasani na wengine wamepata elimu ya ufundi wa namna ya utengenezaji wa Kitalu nyumba.

Mradi huo uliopo sekondari ya Chato mara baada ya kukamilika kwake vijana watakuwa wakipata elimu juu ya kilimo cha kisasa kupitia kwa vijana waliopata mafunzo kwa kushirikiana na idara ya Kilimo ya Halmashauri.

# Kituo cha Mabasi Muganza Chaanza Kujengwa

Halmashauri ya Wilaya ya Chato imeanza rasmi ujenzi wa Kituo kipya cha Mabasi kata ya Muganza.

Fedha za ujenzi wa kituo hicho kipya zimetokana na mkopo wa Shilingi Milioni 100 kutoka benki ya NMB tawi la Chato.

Mradi huo ambao unajengwa kwa kutumia vibarua (Force account) umeanza tangu mwezi Februari 2019 kwa kulipa fidia kiasi cha shilingi milioni 34 kwa wanancnchi waliokuwa wanamiliki eneo hilo lenye ukubwa wa ekari 4.

Afisa Mipango wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato amesema kiasi cha shilingi milioni 66 kilichobaki katafanya kazi ya kusawazisha eneo la kituo cha mabasi, kujenga jingo la abiria pamoja na choo kazi ambazo zinaendelea kwa sasa na inatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2019



*Picha kushoto ni Wajumbe wa kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira wakikagua maendeleo ya ujenzi wa kituo cha mabasi cha Muganza*

## Rubondo Sekondari Kupunguza Msongamano wa Wanafunzi Kigongo

Rubondo sekondari ni shule mpya inayotarajiwa kufunguliwa hivi karibuni wilayani Chato kata ya Kigongo kijiji cha Kikumbaitale.

Kutokana na msongamano mkubwa wa wanafunzi kwenye sekondari ya Kigongo na umbali kutoka Kikumbaitale na mahali ilipo Shule ya sekondari Kigongo ni sababu ya kuanzisha shule hiyo.

Sekondari ya kata ya Kigongo kwa sasa ina jumla ya wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne wapatao 1290.

Kwa mujibu wa Afisa Elimu Sekondari amesema shule hiyo tayari imeombewa usajili wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia mara baada ya vigezo vya awali vya ukaguzi kuwa vimekamilika vizuri.

Shule hii ambayo imejengwa kwa nguvu za wananchi na ufadhili wa TANAPA kupitia hifadhi ya Kisiwa cha Rubondo, kwa sasa shule hiyo ina vyumba 6 vya madara, matundu 10 ya vyoo, ofisi ya walimu na samani za madarasa na ofisi ya walimu ambavyo vinatosheleza mahitaji ya kuanzisha shule mpya kijijini hapo.

Shule zingine ambazo zipo mbioni kukamilika na kuombewa usajili ni pamoja na Sekondari mpya ya Nyabugera iliyopo kata ya Muganza na Sekondari ya Minkoto iliyopo katika kata ya Minkoto ambayo tangu kuanzishwa kwake haikuwa na sekondari ya kata.

Kukamilika kwa usajili wa shule ya sekondari Rubondo, Wilaya ya Chato itafikisha shule za sekondari za serikali 26.

*Vyumba vya madarasa na ofisi ya walimu shule ya sekondari Rubondo kwa ufadhili wa TANAPA*



UCHAGUZI SERIKALI ZA MITAA

2019

Ndugu mwananchi 2019 ni mwaka wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa

Jitokeze kugombea katika ngazi mbalimbali na kuchagua viongozi wenye sifa katika ngazi za Mitaa/ Vijiji na Vitongoji

# HABARI KATIKA PICHA

CHATO yetu Januari-Machi 2019



*Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango wakiwa kwenye ziara ya kukagua ujenzi wa Nyumba sita za walimu shule ya sekondari Ilemela zenye thamani ya shilingi milioni 152 kwa ufadhili wa TEA*



*Wajumbe wa kamati ya Fedha, wakiongea na wanafunzi wa sekondari ya Mnekezi ambao wamekuwa wakitumia maji ya kisima ambayo si salama na badala yake watumie yale ya kisima kilichochimbwa na serikali ambacho kipo maeneo hayohayo*




*Wajumbe wa Kamati ya Fedha wakikagua ujenzi wa madarasa 3 na matundu 13 ya vyoo shule ya Msingi Mnekezi fedha za EP4R 2017*



*Wajumbe wa Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira (hawapo pichani ) walipowatembelea Wafanyabiashara wasoko la kimataifa la Kasenda kujua changamoto zinazowakabili*



*Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Profesa Joyce Ndalichako (wa katikati walio keti)akiwa kwenye picha ya pamoja na walimu wa shule ya sekondari Jikomboe alipowatembelea wakati wa ziara yake kwa ajili ya kuwapongeza kufuatia matokeo mazuri ya shule hiyo*



*Baadhi ya wakurugenzi, Makatibu Tawala wa Wilaya na Maafisa Mipango wa Halmashauri za mkoa wa Geita walipofanya ziara wilayani hapa kwa lengo la kujifunza miradi mikakati iliyoanzishwa na Halmashauri ya Chato*

# HABARI KATIKA PICHA






*Waziri wa Afya, Mendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mhe. Ummy Mwalimu akiangalia mashine ya X-RAY iliyopo katika hospitali ya Wilaya ya Chato wakati wa ziara ya siku moja Wilayani hapa*



*Naibu waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira na Walemavu Mhe. Stela Ikupa (kushoto) akijadili jambo na baadhi ya walemavu wakati wa ziara yake Wilayani hapa mwezi Februari 2019*



*Mkuu wa Wilaya ya Chato Eng. Mtemi Msafiri (wa katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na viongozi na Wilaya na vikundi vya wajasariamali vya walemavu mara baada ya kukabidhi*



*Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato Mhe.Christian Manunga (wa pili kutoka kulia) akiwa kwenye picha ya pamoja na viongozi wa baraza la watu wanaoishi na VVU Tanzania waliponfanya kikao na umoja wa vijana waishio na VVU Wilaya ya Chato*



*Waziri wa Nishati na Mbunge wa Jimbo la Chato Mhe. Dkt. Medard Kalemani (mwenye miwani) akikagua maendeleo ya ujenzi wa kituo kipya cha mabasi kinachojengwa kijiji cha Kahumo kata ya Muungano na kampuni ya Mayanga Construction kwa gharama ya shilingi Bilioni 5.3*




*Balozi wa Marekani nchini Tanzania Dkt. Inmi Patterson(wa pili kutoka kushoto) akiwa na viongozi wa Wilaya ya Chato alipofanya ziara wilayani hapa yenye lengo la kujionea kiwango cha maambukizi hususan katika maeneo ya machimbo*

## Kamati ya Uchumi Yakagua Miradi, Washauri Soko la Kasenda liboreshwe

Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Chato imefanya ziara yenye lengo la kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Baadhi ya wajumbe wa kamati hiyo wameshauri kufanyike maboresho ya haraka hususan kwenye miradi ambayo imeanziswa kwa lengo la kuongeza mapato likiwemo soko la kimataifa la Kasenda

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato Mhe. Christian Manunga akiwa kwenye mradi wa Soko la kimataifa la Kasenda amemwagiza Mkurugenzi Mtendaji kuhakikisha anatengeneza mazingira mazuri katika soko hilo ikiwa ni pamoja na kuziba mashimo yaliyopo katikati ya soko hilo pamoja na utatuzi wa changamoto mbalimbali zinazowakabili wafanyabiashara katika soko hilo.



Soko la Samaki la Kimataifa la Kasenda

Mjumbe wa kamati Mhe. Phares Luhangija ambaye ni diwani wa kata ya Ilyamchele amesema wamefurahishwa na miradi hususan ule wa Ufyatuaji wa Matofali na kuishauri timu ya Menejimenti iweze kufyatua tofali zenye ubora lakini pia kwa gharama nafuu ili kila mwananchi na taasisi ziweze kununua tofali hizo na mradi uwe endelevu.

Miradi mingine iliyotembelewa na kamati hiyo ni pamoja na ujenzi wa kituo kipya cha mabasi cha Muganza pamoja na ujenzi wa uwanja wa mpira wa miguu

# TUNATEKELEZA



## Mpya wa Kituo cha Afya Bwanga Baada ya Ukarabati

**Gharama za Mradi = 500,000,000/=**

**Kituo kinahudumia wananchi 200 kwa siku**

**Zaidi ya wananchi 60,000 wanakitegemea kituo**










## Nyambogo na Idoeselo Kunufaika na Madarasa, Madawati na Vyoo

Shule ya Msingi Nyambongo iliyopo kata ya Ilemela na Idoselo ya kata ya Kachwamba wilayani hapa zinatarajia kunufaika na miundombinu mipya kutokana na serikali ya Japan kufadhili ujenzi wa Vyumba vya madarasa, samani na matundu ya vyoo katika shule hizo.

Akiongea katika Hafla ya kutia saini mkataba wa makubaliano ya ujenzi huo uliofanyika hivi karibuni katika ofisi za ubalozi wa Japan jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato Eliurd Mwaiteleke ameshukuru serikali ya Japan kupitia ubalozi wake nchini Tanzania kwa kuwezesha upatikanaji wa miundombinu hiyo mipya katika shule husika na kusema kiasi hicho cha shilingi milioni 196 kitasaidia kuboresha taaluma katika shule husika.

Fedha hizo zinatarajiwa kujenga vyumba vitatu vya madarasa, matundu ya vyoo na madawati katika kila darasa litakalo jengwa katika shule hizo.



*Balozi wa Japan nchini Tanzania Shinichi Goto (wa pili kutoka kulia) wakikabidhiana nyaraka za makubaliano za ufadhili wa ujenzi wa miundombinu ya elimu katika shule za Nyambogo na Idoselo na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato Eliurd Maiteleke (kushoto) jijini Dar es salaam*

## Kuelekea Uchaguzi TAKUKURU Yawapiga Msasa Wenye Ulemavu

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilayani Chato imetoa elimu juu ya kupambana na rushwa katika sekta mbalimbali kwa watu wenye ulemavu waliopo Wilayani hapa.

Akifungua semina hiyo Seleman Tajiri kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Chato amesema, kundi la watu wenye ulemavu ni mhimu kutokana na wao kuwa sehemu ya jamiii na wamekuwa wakishiriki katika shughuli mbalimbali za miradi ya maendeleo pasipo kujua kwa kina madhara yatokanayo na rushwa.

Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Chato Vangsada Mkalimoto amesema TAKUKURU imeamua kutoa semina kwa kundi hilo kutokana na wao kundi hilo kuwa sehemu ya mapambano ya rushwa kwenye jamii kwani ni kundi mojawapo ambalo limekuwa likiatirika na rushwa kupitia maeneo mbalimbali wanayojihusisha nayo.




Kwa upande wake katibu wa Taasisi ya Maendeleo ya Viziwi Tanzania (TAMAVITA) Calvin Mnyema amesema mafunzo hayo yametolewa kutokana na viziwi wengi kutokufahamu namna ya kupambana na rushwa sababu ambayo imepelekea baadhi yao kuchagua hata viongozi wasio na sifa katika chaguzi mbalimbali.

Justine Lupande ambaye ni mlemavu wa viuongo amesema kutokana na elimu hiyo waliyopata itawasaidia kupambana na rushwa hususan katika kipindi hiki cha kuelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa.

Mafunzo hayo ya siku moja yalilenga kuwajengea uwezo walemavu wa namna ya kupambana na rushwa hususan kwenye miradi ya maendeleo, chaguzi za kisiasa, elimu ya uraia katika upatikanaji wa haki, maeneo ya kutolea huduma mbalimbali, haki za raia mbele ya jeshi la polisi.

# Waziri Mwalimu avutiwa na Ukarabati Hospitali ya Wilaya

Waziri wa afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Ummy Mwalimu amesifu utoaji wa huduma bora katika hospitali ya Wilaya Chato na ameuagiza uongozi kutenga chumba maalumu kwa ajili ya wagonjwa wa dharula ili kuokoa mamia ya watu ambao wamekuwa wakipata ajali mbalimbali na chumba cha uangalizi wa watoto wachanga mahututi ili kupunguza vifo vya watoto.

Waziri Mwalimu ameyasema hayo hivi karibuni wakati wa ziara yake ya siku moja aliyoifanya katika Wilayah ii kwa lengo la kujionea utoaji wa huduma katika hospitali ya Wilaya ya Vituo vya afya.

Katika hatua nyingine Waziri Mwalimu ameupongeza uogozi wa Hospitali kwa kukarabati majengo yaliyopo hospitalini kwa kutumia fedha za RBF kiasi cha shilingi milioni 65 ambapo amesema ukarabati huo umependezesha mwonekano hata kuwafanya wagonjwa wajiskie vizuri kutonana na mandhari nzuri iliyopo hospitalini hapo.

"hata mgonjwa akija akiona hospitali kuna rangi nzuri hata ugonjwa unaanza kupungua na mimi nimefurahi sana hata wafadhili wetu wakiona watafurahi pia" alisema waziri Mwalimu





# Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha afya kata ya Muganza





Picha hapo juu ni mwonekano wa baadhi ya majengo ya kituo cha Afya cha kata ya Muganza. Kituo hiki kinajengwa kwa gharama ya shilingi milioni 400 zilizotolewa na serikali kupitia ofisi ya Rais TAMISEMI. Kituo hiki cha afya kitakuwa na jengo la upasuaji, wodi wa wazazi, chumba cha maiti, jengo la Maabara na nyumba 2 za watumishi ambapo kwa kutumia njia ya vibarua Halmashauri imeongeza majengo mengine mawili likiwemo la kufua nguo na wodi ya akina mama .

Kituo hicho cha afya ambacho kinatarajiwa kukamilika mwezi Mei 2019 kitasaidia zaidi ya wananchi elfu 40 wa kata za Muganza, Bwongera na maeneo jirani na kata hizo.

# Mwenge wa Uhuru 2019 Wilayani Chato Tar. 2 Mei

Mwenge wa Uhuru utakimbizwa Wilayani Chato tarehe 2 Mei 2019.

Mwenge wa Uhuru 2019 utapokelwa wilayani Chato siku Alhamis tarehe 2 Mei katika viwanja vya shule ya msingi Ichwankima ukitokea wilayani Biharamulo.

Ukiwa Wilayani hapa Mwenge wa uhuru unatarajiwa kuweka jiwe la Msingi kwenye ujenzi wa nyumba sita za walimu sekondari ya Ilemela, kuzindua barabara ya lami Chato mjini, kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa kituo cha afya cha Bwina, kutembelea klabu ya wapinga rushwa shule ya msingi Nyabilezi.

Miradi mingine itakayopitiwa na Mwenge wa Uhuru 2019 ni pamoja na kuzindua kisima kirefu cha maji kijiji cha Busaka kata ya Bwera, kutoa mikopo kwa vikundi vya wenye ulemavu, vijana na wanawake pamoja na kutembelea mabanda ya upimaji UKIMWI, Malaria, Uchangiaji wa damu na mabanda ya kupinga madawa ya kulevya katika eneo la mkesha Buseresere na tarehe 3 Mei Mwenge utakabidhiwa Wilayani Bukombe.



Nyumba sita za walimu sekondari ya Ilemela ambazo zitawekewa jiwe la msingi na mwenge wa uhuru 2019

# Vikundi 21 Vyanufaika na Mikopo ya Mikopo Isiyo na Riba

Jumla ya vikundi 21 vya vijana, Wanawake na walemavu kutoka maeneo mbalimbali ya Halmashauri ya Wilaya ya Chato vimenufaika na mikopo isyokuwa na riba inayotolewa na Halmashauri kupitia fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri.

Akikabidhi mikopo hiyo yenye thamani ya shilingi milioni 39 Mkuu wa Wilaya ya Chato Mhandisi Mtemi Msafiri Simeon amevishauri vikundi hvyo kutumia kwa uangalifu fedha hizo ili badae vikopeshwe tena fedha zaidi ya hizo walizokopeshwa kwa awamu hii.

Katibu wa UWT Wilaya ya Chato Cecilia Ismail amesema vikundi vilivyopata mikopo kwa awamu hiyo vinapaswa kujitahidi kutumia fedha hizo kwa malengo ambayo wamejiwekea na kuongeza kusema kuwa wanavikundi hao katika kazi zao wanatakiwa kuwa mabalozi wazuri katika ulipaji wa kodi na kuwashawishi watanzania wengine wapende kulipa kodi ili serikali iweze kurahisisha upelekaji wa maendeleo kwa wananchi wake.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato Eliurd Mwaiteleke amesema fedha izo zinazotolewa na Halmashauri ni fedha za mapato ya ndani na ukusanyaji wa mapato ukienda vizuri kwa mwaka huu wa fedha fedha ambazo zitatolewa zitakuwa ni milioni 220 ambapo hadi sasa jumla ya shilingi milioni 84 zimekwisha tolewa kwa vikundi mbalimbali vilivyopo wilayani hapa.

Mwezi Julai 2018 Halmashauri ya Wilaya ya Chato ilitoa milioni 45 kwa vikundi 27 vya vijana, wanawake na walemavu.

Halmashauri ya Wilaya ya Chato ina vikundi 763 vilivyosajiliwa ambavyo vinakadiriwa kuwa na wanachama 11,445.



*Picha ya Kwanza hapo juu Mkuu wa Wilaya ya Chato Mhandisi Mtemi Msafiri akikabidhi nakala ya uthibitisho wa malipo kwa mwakilishi wa kikundi cha walemavu kata ya Nyarutembo Boniphace Thomas na picha kushoto ni viongozi wa Wilaya wakiwa kwenye picha ya pamoja na wanavikundi walionufaika na mikopo*

# CHATO yetu

TOLEO NAMBA 17 JANUARI HADI MACHI 2019


## Uwanja wa Mpira Chato Mambo ni Moto

**Huu Ndio Mwonekano wa Hali halisi ya uwanja hadi sasa**

**Sehemu ya kuchezea mpira kukamilika mwezi Juni 2019**



Maendeleo ya uwanja Mkubwa na wa kisasa Wilayani Chato umepamba moto mara baada ya nyasi zilizopandwa uwanjani hapo kuanza kuota hivyo kuleta matumaini mapya kwa wanamichezo wa Chato.

Hivi sasa kazi ya kukuza nyasi kwenye eneo la kuchezea unaendelea sambamba na ung'oaji wa magugu.

Kwa mujibu wa mtaalamu wa nyasi anasema itachukua takribani miezi 2 kutoka sasa ili sehemu ya kuchezea ikamilike.

Uwanja huu uliopo kata ya Muungano kijiji cha Mlimani unajengwa kwa ufadhili wa Benki ya CRDB ambao walitoa zawadi kwa Wilaya Chato kupitia kwa Mhe. Rais John Pombe Magufuli alipokuwa anazindua tawi jipya la benki hiyo mwezi Machi mwaka 2018.



*Katibu wa UWT Wilaya ya Chato ndugu Cecilia Ismail akijumuika kucheza na kikundi cha Mwagazege kwenye maadhimisho ya siku ya wanawake Duniani yaliyofanyika kiwilaya kata ya Nyamirembe*